

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI
WAKALA WA VYUO VYA MAFUNZO YA MIFUGO



KUPE NA ATHARI ZAKE KWA MIFUGO

Kimetayarishwa na:

Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA)
Kampasi ya Morogoro
S.L.P. 603,
MOROGORO – TANZANIA
E-mail: litamorocamp@gmail.com

UTANGULIZI

Magonjwa ya mifugo yanayoenezwa kwa kupe huathiri maendeleo ya ufugaji kwa kiasj kikubwa nchini Tanzania. Kupe na wadudu wengine hutegemea damu ya wanyama ili waishi. Na kwa njia hii hueneza vijidudu vya magonjwa ambapo ni moja kati ya vikwazo vikubwa vya uzalishaji wa mifugo nchini.

MAGONJWA HATARI YANAYOENEZWA NA KUPE

- Ndigana kali: East Coast Fever
- Ndigana baridi: Anaplasmosis
- Kukojoa damu: Babesiosis
- Maji moyo: Heart water
- Kuvimba bandama: Canine Ehrlichiosis

JINA LA KUPE NA UGONJWA ANAOSABABISHA

- *Ripicephalus appendiculatus* – Ndigana kali (ECF) kwa ng'ombe
- *Boophilus Sp.*- Ndigana baridi (kwa ng'ombe) na Kukojoa damu (kwa ng'ombe)
- *Amblyoma sp.* Maji moyo kwa ng'ombe, mbuzi na Kondoo
- *Hyaloma sp.* Kukojoa damu (kwa Farasi na Punda)
- *Ripicephalus sanguineus* Kuvimba bandama (kwa mbwa.)

BAADHI YA VIFAA VINAVYOTUKA KUDHIBITI KUPE:

- Kinyunyizi mbereko (Knapsack sprayers)
- Nyunyiza kwa ndoo (Bucket sprayers)
- Nyunyiza kwa pampu ya umeme (Spray races)
- kuogelea kwenye joshu (dipping)

BAADHI YA DAWA ZITUMIKAZO KUUA KUPE

1. Paranex^(R)- Alpha Cypermethrin 10% EC
2. Drop on^(R) – Deltamethrin 1% pour on.
3. ECOTIX 10% EC (Cypermethrin high cis
4. Tik Tik^(R) – Amitraz 12.5% EC

NDIGANA KALI: (EAST COAST FEVER)

Husababishwa na vijidudu viitwavyo *Theileria Parva* na hushambulia sana chembechembe nyeupe za damu.

Huenezwa na kupe aina ya **Ripicephalus appendiculatus**

DALILI MUHIMU: -

Homa kali kufikia digrii 42 za joto, Mnyama kuacha kula, Kupumua kwa shida, Kuvimba tezi, na Kutembea kwa shida.

UCHUNGUZI BAADA YA KIFO:

Povu kwenye njia za hewa na mapafu; Kuvimba kwa tezi, ini, figo, moyo n.k. Madoadoa meupe kwenye figo na madoadoa mekundu kwenye moyo, ulimi, utumbo, figo.

TIBA:

Tumia dawa zifuatazo:
Parvaquone+Oxtetracycline LA+frusemide+multivitamin

KINGA:

Tumia dawa za kuua au kupunguza kupe mara kwa mara kwa mfano: kuosha mifugo, kufuga mifugo kwa ndani na Wapatie ng'ombe chanjo

NDIGANA BARIDI: (ANAPLASMOSIS, GALL SICKNESS)

DALILI MUHIMU:

Homa kali – kufikia digrii 41.5 za joto, Upungufu wa damu mwilini, Umanjano.

Kinyesi kigumu, Mwili kudhoofu na Kutopenda kula .

Mabadiliko katika maumbile ya chembechembe hizo (Hypochromasia, anusocystosis etc)

TIBA

Tumia oxytetracycline, Kuongeza damu kwa sindano (Iron injection) au Kutumia dawa iitwayo Imidocarb dipropionate.

KINGA

Tumia dawa za kuangamiza kupe mara kwa mara

KUKOJOA DAMU (BABESIOSIS, REDWATER):

Husababishwa na vijidudu viitwayo Babesia Sp.
Huenezwa na kupe waitwao Boophilus Sp.

DALILI MUHIMU:

Upungufu wa damu (anaemia), Mnyama Kukojoa damu (ng'ombe), Kupumua kwa shida, na Homa kali kufikia digrii 42 za joto

UCHUNGUZI BAADA YA KIFO

Maji mengi kwenye moyo, Bandama kuvimba na Maji kwenye mapafu

TIBA:

Tumia dawa itwayo oxytetracycline. Au Imizol

KINGA:

Tumia dawa za kupe mara kwa mara.